# Hagai

### *Wito wa kujenga Hekalu*

1 Katika mwaka wa pili wa utawala wa Mfalme
Dario, katika siku ya kwanza ya mwezi wa sita,
neno la Mwenyezi Mungu lilikuja kupitia kwa
nabii Hagai kwenda kwa Zerubabeli mwana wa
Shealtieli, mtawala wa Yuda, na kwa Yoshua*
mwana wa kuhani mkuu Yehosadaki:
2 Hivi ndivyo asemavyo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni: “Hawa
watu husema, ‘Wakati haujawadia wa kujenga
nyumba ya Mwenyezi Mungu.’ ”
3 Kisha neno la Mwenyezi Mungu likaja kupitia
kwa nabii Hagai:
4 “Je, ni wakati wenu ninyi wa kuishi katika
nyumba zenu zilizojengwa vizuri, wakati hii
nyumba ikibaki gofu?”
5 Sasa hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni: “Zitafakarini
vyema njia zenu.
6 Mmepanda vingi, lakini mmevuna haba.
Mnakula lakini hamshibi, mnakunywa, lakini
hamtosheki. Mnavaa nguo, lakini hamsikii
joto. Mnapata mishahara, lakini inatoweka kama
imewekwa kwenye mfuko uliotobokatoboka.”

* **1:1** kwa Kiebrania ni *Yeshua*, maana yake *Yehova ni wokovu*

7 Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: "Zitafakarini vyema
njia zenu.
8 Pandeni milimani mkalete miti na kujenga
nyumba, ili nipate kuifurahia, na nitukuzwe,"
asema Mwenyezi Mungu.
9 "Mlitarajia mengi, kumbe, yametokea kidogo.
Ulichokileta nyumbani nilikipeperusha. Kwa
nini?" asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni. "Ni kwa sababu ya nyumba
yangu, inayobaki katika hali ya magofu, wakati
kila mmoja wenu anajishughulisha na nyumba
yake mwenyewe.
10 Kwa hiyo, mbingu zimezuia umande wake
na ardhi mavuno yake kwa sababu yenu.
11 Niliita ukame mashambani na milimani,
kwenye nafaka, mvinyo mpya, mafuta pamoja na
chochote kinachozalishwa na ardhi, juu ya watu
na ng'ombe, pamoja na kazi za mikono yenu."

12 Kisha Zerubabeli mwana wa Shealtieli,
Yoshua kuhani mkuu mwana wa Yehosadaki,
pamoja na mabaki yote ya watu wakaitii sauti
ya Mwenyezi Mungu, Mungu wao, pamoja na
ujumbe wa nabii Hagai, kwa sababu alikuwa
ametumwa na Mwenyezi Mungu, Mungu wao.
Watu walimwogopa Mwenyezi Mungu.
13 Kisha Hagai, mjumbe wa Mwenyezi Mungu,
akawapa watu ujumbe huu wa Mwenyezi
Mungu: "Mimi niko pamoja nanyi," asema
Mwenyezi Mungu.
14 Kwa hiyo Mwenyezi Mungu akachochea
roho ya Zerubabeli mwana wa Shealtieli,

mtawala wa Yuda, na roho ya kuhani mkuu Yoshua mwana wa Yehosadaki, pamoja na roho za mabaki yote ya watu. Walikuja, wakaanza kufanya kazi katika nyumba ya Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni, Mungu wao,

15 siku ya ishirini na nne ya mwezi wa sita, katika mwaka wa pili wa utawala wa Mfalme Dario.

# 2

### *Utukufu ulioahidiwa wa Hekalu jipya*

1 Katika siku ya ishirini na moja ya mwezi wa saba, neno la Mwenyezi Mungu lilikuja kupitia nabii Hagai, kusema:

2 “Sema na Zerubabeli mwana wa Shealtieli, mtawala wa Yuda, kuhani mkuu Yoshua mwana wa Yehosadaki, na mabaki ya watu. Uwaulize,

3 ‘Ni nani miongoni mwenu aliyebaki ambaye aliiona hii nyumba katika utukufu wake wa mwanzo? Sasa inaonekanaje kwenu? Je, haionekani kwenu kama si kitu?

4 Lakini sasa uwe imara, ee Zerubabeli,’ asema Mwenyezi Mungu. ‘Kuwa imara, ee kuhani mkuu Yoshua mwana wa Yehosadaki. Mwe imara, enyi watu wote wa nchi,’ asema Mwenyezi Mungu, ‘na mfanye kazi. Kwa kuwa mimi nipo pamoja nanyi,’ asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.

5 ‘Hili ndilo nililoagana nanyi mlipotoka katika nchi ya Misri. Pia Roho wangu Mtakatifu anadumu kati yenu. Msiogope.’

6 “Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu, Mungu
wa majeshi ya mbinguni: ‘Baada ya muda kidogo
kwa mara nyingine nitazitikisa mbingu na nchi,
bahari na nchi kavu.
7 Nitatikisa mataifa yote, nacho kile kinachota-
maniwa na mataifa yote kitakuja, nami nitaujaza
utukufu katika nyumba hii,’ asema Mwenyezi
Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni.
8 ‘Fedha ni mali yangu na dhahabu ni mali
yangu,’ asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni.
9 ‘Utukufu wa nyumba hii ya sasa utakuwa
mkubwa kuliko utukufu wa ile nyumba ya
mwanzoni,’ asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni. ‘Na mahali hapa nitawapa
amani,’ asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa
majeshi ya mbinguni.”

## *Baraka kwa watu waliotiwa unajisi*

10 Katika siku ya ishirini na nne ya mwezi
wa tisa, katika mwaka wa pili wa utawala wa
Dario, neno la Mwenyezi Mungu lilikuja kwa
nabii Hagai:
11 “Hili ndilo asemalo Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni: ‘Ulizeni
makuhani jinsi sheria inavyosema:
12 Kama mtu akibeba nyama iliyowekwa wakfu
katika pindo la vazi lake, kisha lile pindo lika-
gusa mkate au mchuzi, divai, mafuta au chakula
kingine, je, kitu hicho kitakuwa kimewekwa
wakfu?’ ”

Makuhani wakajibu, “La.”

13 Kisha Hagai akasema, “Je, kama mtu
aliyetiwa unajisi kwa kugusa maiti akigusa
mojawapo ya vitu hivi, kitu hicho kitakuwa
kimetiwa unajisi?”

Makuhani wakajibu, “Ndiyo, huwa kimena-
jisiwa.”

14 Kisha Hagai akasema, “ ‘Basi ndivyo walivyo
machoni pangu hawa watu na taifa hili,’ asema
Mwenyezi Mungu. ‘Lolote wafanyalo na cho-
chote watoacho hapo ni najisi.

15 “ ‘Sasa fikirini kwa uangalifu kuanzia leo na
kuendelea: tafakarini jinsi mambo yalivyokuwa
kabla halijawekwa jiwe moja juu ya lingine
katika Hekalu la Mwenyezi Mungu.
16 Mtu alipoendea lundo la nafaka la vipimo
ishirini, kulikuwa na vipimo kumi tu. Mtu
alipoendea pipa la mvinyo ili kuchota vipimo
hamsini, kulikuwa na vipimo ishirini tu.
17 Kazi zenu zote za mikono nilizipiga kwa
ukame, ukungu na mvua ya mawe, lakini hata
hivyo, hamkunigeukia mimi,’ asema Mwenyezi
Mungu.
18 ‘Tangu leo na kuendelea, kuanzia siku hii ya
ishirini na nne ya mwezi wa tisa, tafakarini siku
ambayo msingi wa Hekalu la Mwenyezi Mungu
uliwekwa. Tafakarini:
19 Je, bado kuna mbegu iliyobakia ghalani?
Hadi sasa, hakuna mzabibu au mtini, mkoma-
manga wala mzeituni uliozaa tunda.

“ ‘Kuanzia leo na kuendelea, nitawabariki.’ ”

### *Zerubabeli pete ya muhuri ya Mwenyezi Mungu*

20 Neno la Mwenyezi Mungu likamjia Hagai
kwa mara ya pili katika siku ya ishirini na nne
ya mwezi kusema:
21 "Mwambie Zerubabeli mtawala wa Yuda
kwamba nitazitikisa mbingu na nchi.
22 Nitapindua viti vya falme, na kuziharibu
kabisa nguvu za falme za kigeni. Nitapindua magari ya vita pamoja na waendeshaji wake; farasi
na wapanda farasi wataanguka, kila mmoja kwa
upanga wa ndugu yake.
23 " 'Katika siku ile,' asema Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni, 'nitakuchukua wewe, mtumishi wangu Zerubabeli mwana wa Shealtieli,' asema Mwenyezi Mungu. 'Nitakufanya kama pete yangu ya muhuri, kwa kuwa nimekuchagua,' asema Mwenyezi Mungu, Mungu wa majeshi ya mbinguni."

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: “Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible.”

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

“Biblica” ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

“Biblica” is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.

If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025

72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d